

Naila S. Kharusi  
1966  
USINISAHAU  
Swahili, Vol. 36/2, S.56-80  
Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research

Nacherzählt von  
Lourenco Noronha

Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur  
am  
Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien  
Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika  
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: Mai 2009

Widmung  
*Kutabaruku*

al-hamdu li-llahi  
subhanahu wa-ta'ala

## 1. Einleitung

Usinisahau ist ein Frühwerk der Post-Uhuru Literatur auf Kiswahili, das vom bleibenden Wert ist. Diesen Kurzroman<sup>1</sup> in der ersten Person rückwirkend erzählt, der gut durchgedacht und kompakt ist, empfehle ich auch als ein Musterbeispiel von Swahili-Literatur von einer Frau verfasst. Ich beziehe es auf die Frauen-Sprache, die gefühlvolle psychologische Erzählweise und die Thematik. Es ist empfehlenswert, diesen Kurzroman in Zusammenhang mit Kurwa na Doto von Saleh Farsi zu lesen. Usinisahau veröffentlicht in 1966, bewegt sich in der Welt der oberen Gesellschaftsschicht in Sansibar, worin aber die Neuorientierung nach der Volksrevolution von 11/12. Januar 1964 kaum zu spüren ist.

Die Orthographie von Kharusi Kiswahili weicht gelegentlich von jener der *Kiswahili Sanifu* ab. Ich habe sie jedoch unverändert hier wiedergegeben.

## 2. Matini

*Ich heisse Shadya und wohne in Sansibar. Ich sitze in der Stube meines Elternhauses. Es regnet draussen.*

Maradi ya mimeme iliendelea mpaka karibu ya alfajiri, na hapo mvua kubwa ilianza kunyesha. Kwa kuogopa mpepeo wa mvua usiingie chumbani, niliinuka mbio mbio kufunga madirisha. Hapo naliweza kuuona ulimwengu wa kiza na wa kishindo kabisa machoni mwangu. Kwa muda, nilijibanza pembeni nikiangalia matone ya mvua yaliyokuwa yakipiga kwa nguvu juu ya vioo vya madirisha, na baadaye kufanya michirizi hata ikawa siwezi tena kuyaona ya nje. Na hapo, ijapokuwa usiku wa kucha sikulala kwa vizuri<sup>2</sup> kwa ajili ya ndoto mbayambaya zilizokuwa zikinigutua mara kwa mara, nalijiona kuwa sitamani tena kurejea kitandani. Jitimia na majonzi niliyolala nayo tangu usiku mapema kwa kukumbukia kwamba leo ni siku aliyozaliwa Nadya, sasa nilihisi kuwa yamenizidi mno. Nadya! Ndugu yangu, namna gani ninayomtamani leo hii nimuone. Tuhadithiane tuliyo nayo na yaliyotupitilia katika miaka michache hii tuliyokuwa mbali mbali. Ama kweli mengi yaliyobadilika!!

Taratibu niliwasha taa, nikafungua mtoto wa meza<sup>3</sup> ndogo iliyopo karibu na kitanda, na kutoa buku la kuweka picha ambazo Baba yetu akitupiga tulipokuwa wadogo. Hapo macho yangu upesi mno yalipiga juu ya picha maalum niipendayo kuliko zote. Ghafula tu nilihisi wazi wazi fikira nyingi zinanimimikia za maisha yaliyopita, hata nikawa ninahisi kama kwamba mambo hayo yananitendekeza hivi machoni mwangu wakati huo huo. Ni kweli ninaikumbuka wazi wazi siku tuliyopiga picha hii, mimi na Nadya. Ilikuwa ni siku kama ya leo; siku ya tarehe ya kuzaliwa kwake Nadya.

Baada ya Baba kutupiga picha nyingi pamoja na shoga zetu, alipiga picha hii ya ghafula, wakati tulipokumbatiana kwa furaha mimi na ndugu yangu, nilipompa zawadi yake. Hii ni picha ielezayo hasa mapenzi ya ndugu – mapenzi ya kitoto, nadhifu na ya kweli kabisa

---

<sup>1</sup> Ki-riwaya

<sup>2</sup> „Sikulala vizuri“ wäre mir lieber.

<sup>3</sup> Schublade

kabisa. Namna gani alivyopendeza Nadya siku ile! Alipokuwa ndani ya bustani yetu ya maua ya kila rangi akawa kama kipepeo cha peponi miongoni mwa watoto wengineo! Akirukaruka kwa furaha huku nywele zake za rangi ya kahawia zikipigapiga juu ya kanzu yake ya lesi nyeupe. Oh! Alikuwa ni kitu kizuri mno cha kukitazama. Na baada ya kukusanyika sote pale mezani penye keki yake kubwa nyeupe yenye urembo wa waridi, ambayo kwa muda wa siku tatu mbele Mama alikuwa akiitengeneza na kuipamba; naliona kwamba Nadya hadi ni mtoto ambaye aliyebahatika kwa yote.

Ngozi changa laini ya uso wake iliwiva, na macho yake yaliyo makubwa meusi yenye makope marefu mweusi, yaling'ara zaidi kwa nuru ya mishumaa minane iliyokuwa pale mbele yake tayari kuizima. Baada ya watoto kumshangilia kwa nyimbo na makofi, Mama aliyekuwa pembeni, alimhimza Nadya awakaribishe vyakula wageni wake, lakini Nadya alimjibu, "Aah! Mama, siwezi hayo. Ninataka kwenda cheza dansa; mwambie Shadya aandikie." Na Mama alisema, "Vyema mwanangu. Nenda kafurahi, kwani leo ni siku yako ya furaha, na kweli usihangaika Shadya yupo atatumika.

Nami kabla Mama hajanipa kombe la sambusa kuwapitishia wageni, nilimuomba anisubiri kidogo, nakamwita, "Nadya, shika zawadi hii ndogo inayotoka kwangu." Alipotupa jicho na kuiona zawadi ni ipi mara alinikumbatia kwa nguvu na kusema, "Ah Shadya! Asante sana, ahsante sana. Ama hata sijui nikwambie vipi nilivyofurahi! Hiki hasa ndicho kitu nilichokuwa nikikitamani niwe nacho. Hebu tazama ilivyonipendeza mkononi mwangu." Zawadi yenyewe ilikuwa ni bangili ya fedha iliyokuwa ina nakshi ya maandishi: "Usinisahau." Tuliiona pamoja dukani, na Nadya aliipenda sana. Kwa hivyo, nilidunduliza pesa kwa siri za kumnunulia ili nimpe siku ya leo. (Uk. 56-57).

*Nadya war zwei Jahre jünger als ich, aber da wir beide ähnliche Kleider trugen, sahen wir wie Zwillinge aus. Vom Charakter her war Nadya fröhlich und unternehmungslustig. Schon beim ersten Anblick konnte man sich in sie verlieben. Auch ich hatte sie gern. Sie half mir auch einige Mal die Strafe der Mutter zu entrinnen, wenn ich unartig war, denn sie wusste genau, wie man unsere Mutter besänftigen kann.*

*Eines Abends als meine Mutter bei einer Hochzeitsfeier war, spielten Nadya und ich fangeln in einem Zimmer, in dem es uns verboten war zu spielen. Beim Rennen stiess ich auf einem Tisch und warf eine Blumenvase herunter, die zerbrach. Ich war erschrocken und voller Angst, denn meine Mutter liebte diese Vase sehr. Nadya dagegen spaste, als ob nichts geschehen wäre. In diesem Augenblick öffnete unsere Mutter die Türe und kam herein. Ich lief die Stiege hinauf und versteckte mich. Die Mutter sagte überrascht: „Meine Vase ist zerbrocken. Wer hat es getan?“ Nadya teilte ihr mit, dass sie es war und beschrieb, wie es geschehen war. Die Mutter nahm es gelassen und schickte Nadya schlafen, während sie selbst die Scherben zusammenkehrte. Unsere Mutter liebte Nadya sehr und Nadya wusste, dass sie alles tun darf, ohne dass, die Mutter sich ärgern würde.*

Ninakumbuka siku moja ya Sikukuu, Baba yetu alituchukua<sup>4</sup> dukani kutununulia michezo; Nadya upesi alichagua mtoto wa sanamu mkubwa na aliye mzuri kuliko wote hapo, na ndiyo baadaye na miye nikawaza kuchagaua katika waliobakia. Tulipofika nyumbani,

---

<sup>4</sup> Anglizismus „took us“

Nadya alimongwa mtoto wake, akameguka kidogo sana kidole cha gumba cha mguu. Hapo Nadya aligargara chini na vilio visivyokuwa vidogo, akipiga kelele, „Simtaki, simtaki tena mtoto huyo mbovu.” Baba alimbembeleza, na kumwambia kwa taratibu, „Si mbovu, kwani ni kidogo tu amemeguka; mchezee, na siku za mbele nitakununulia mwingine (mwingine).“ Lakini Nadya aliendelea kusema, „Simtaki tena huyu. Ninamataka huyo mdogo wa Shadya – ndiye ninayempenda. Mwambie tubadilishane.“

Hapo Baba alistaajabu, na kumuuliza (kumwuliza), „Lakini ilikuwaje Nadya? Huyu mtoto umemchagua mwenyewe, tena mwanzo kabla ya Shadya kumchagua wake; na vipi sasa amekuwa si mzuri?“ Ghadhabu ilimzidi Nadya, na alisema kwa kelele, „Mimi hayo siyajui, ila mwambie Shadya tubadilishane, au nitalitupa, nilivunjilie mbali toto hili.“ Baba alimjibu kwa taratibu ingawa uso wake ulionesha (ulionyesha) umewiva kwa hamaki, „Mvunje; lakini jua hutompata (hutampata) mtoto wa Shadya wala ye yote mwingine (mwingine) sitokununulia (sitakununulia).“ Kwa hivyo, Shadya alizidi kupiga makelele ya vilio, na kumtupa kwa nguvu mtoto wake juu ya sakafu, akavunjika vipande vipande.

Mama aliyekuwa juu, alishuka kwa haraka, akauliza, „Kuna nini tena jamani? Nadya mwanangu, mbona unalia? Njoo mwanangu, mbona unalia? Njoo mwanangu nikupakate; njoo mpenzi wangu.” Baba alimweleza Mama yote yalivyokuwa, na akamaliza kwa kumuomba (kumwomba), „Bibie, mwachie aliye mwisho atanyamaza.” lakini Mama alinena, „Eh jamani, na ninyi mnapenda makelele – hamumpi (ham-m-pi) huyo mtoto ampendaye?” Na tena alinigeukia mimi, na kuniambia, „Shadaya mwanangu, hebu mridhi mdogo wako – umpe huyo mtoto. Wake ndiyo keshamvunja kwa hamaki, na alivyo mkaidi? Namjua Nadya hanyamazi mpaka apewe anachotaka.” Hapo Baba kwa sauti ya tashtiti aliuliza, „Alaa? Ndivyo ulivyomzoelesha, Bibie? Ni uzuri uliyoeleza; nikapata kujua. Lakini bibie kwa leo hii inafaa ufahamu wewe na yeye Nadya, kwamba kilio chake hakitosaidia (hakitasaidia) kupata anayoyataka, hata akilia kutwa na kucha. Nadya lazima ajifunze kwamba si yote ayatakayo duniani lazima ayapate ijapokuwa si kwa njia nzuri ifaayo. Tena lazima ajifunze kuwafikiria wenzake, siyo nafsi yake tu, kama mnyama. Na la mwisho, ijapokuwa ni mwanzo, yeye aliposema kuwa anampenda na anamtaka mtoto wa Shadya, kwa nini hakujua mbele kama huyo ndiye amtakaye? Mbona hajamchagua tangu mwanzo? Lakini miye sasa nimekwishajua wapi anapotelea Nadya, na kwa hivyo, Bibie, sitakuwachia (sitakuachia) uzidi kumpoteza.”

“Lakini Bwana, Nadya bado mdogo – atajifunza yote hayo wakati wake ukiwadia.” Mama alijibu. „Wakati wake ndio huu wa kujifunza; ni wakati udongo uli maji<sup>5</sup>, siyo ukisha kauka”, Baba alisema. Mradi mzozano uliendelea, na mwishowe nikaona sasa hivi Mama na Baba watagombana. Kwa hivyo, sikuwa na la kufanya; ila niliona hapana njia bora zaidi ila nimsamehe mtoto wangu wa sanamu, nikipenda nisipende. Nilimwangualia mtoto wangu kwa mara ya mwisho, nikamjongelea Nadya, na kumwambia, „Nadya, basi usilie. Shika huyu mtoto unayemtaka; miye haidhuru.” Lakini Baba alipoyaona hayo alisema, „Kwa nini

---

<sup>5</sup> Siehe den Link [Sprichwörter](#) auf dieser Website.

Udongo upatilizite (ukande), uli maji.

Arbeite mit dem Ton während er noch nass ist.

*Bedeutung:* Nutze gute Gelegenheiten!

Shadya? Usimtoe mtoto wako. Mwache tu alie.” “Lakini, Baba, nimekumbuka miye sasa ni mkubwa – naona bora nisichezee tena mtoto wa sanamu”, nikamjibu kwa sauti thabiti, na uso wa ukunjufu. Nilimyakinisha hayo mara mbili mbili mpaka Baba akawa hana ila kuniachia nimpe mtoto Nadya. Na hapo ndipo zahama zikamalizika – na sote tukapumzika. (Uk. 58-59).

*Ich war sehr bedacht, meine Mutter nicht zu kränkeln. Ich war auch ihrer Liebe nie sicher. Während ich mich bemühte, sie nicht zu ärgern, hoffte ich, dass sie mich doch umarmen werde. Ich habe nie verstanden, warum sie Nadya mehr liebte. Vielleicht war es wegen ihrer Schönheit. Meine Mutter konnte ihre Freude nicht verstecken, wenn die Nachbarn Nadyas Schönheit lobten. Sie fügten dann hinzu, dass Nadya ihrer Grossmutter mütterlicherseits, die für ihre Schönheit bekannt war, ähnelte. Ich glich meinem Vater, der gross und schlank war und eine blasse Farbe hatte. Meine Haare sind schwarz wie Ebenholz und ganz gerade. Meine grosse, schwarze Augen sind jenen meines Vaters ähnlich, besonders wenn ich lache. Die Nachbarn nannten uns „die zwei Rosen von Frau Aliya“. Ich war nicht einmal sicher, denn ich war ja nur ein Stern in Nadyas Mondschein<sup>6</sup>.*

*Wenn Gäste auf Besuch kamen, pflegte meine Mutter Nadya zu rufen und sie zu bitten, Klavier zu spielen und zu singen. Auch sonst, wenn wir irgendwo beide gemeinsam hingingen, war Nadya immer der Mittelpunkt. Ich hatte dabei das Gefühl, dass ich die Randfigur bin und vom geringen Wert. Ich wurde immer scheuer und ängstlicher, so dass manchmal sehr ungeschickt in der Gesellschaft anderer Leute verhielt. Diese meine geheime Schwäche und der Wunsch wenigstens meiner Mutter zu gefallen, veranlasste mich fleissig zu studieren. Ich hatte die besten Noten in der Klasse und als ich mein Zeugnis nach Hause brachte, freuten sich alle. Diese Freude dauerte aber nur kurze Zeit.*

Safari moja skuli (shuleni) nilipewa zawadi ya kalamu nzuri kwa ajili ya kufuzu kwangu. Nilirudi nyumbani kwa hamu kubwa ya kumfurahisha Mama.

Mama! Mama! Uko wapi? Njoo nikuonyeshe kitu kizuri, utafurahi sana.” Nilimpigia kelele nilipoingia tu nyumbani. Na alinijibu, “Nipo jikoni, Shadya. Njoo huku.”

“Mama tazama nimepewa skuli sababu nimetokea wa mwanzo katika klasi (darasa letu) yetu”, nilimwambia na huku ninautizama (ninautazama) uso wake vipi utavyobadilika. Mama alipoiona ni kalamu, alisema, “Si mbaya, itakufaa kuandikia, mwanangu. Jee (je) ndugu yako naye kapewa?” Nilipomjibu hakupewa alifazaika (alifadhaika) na akasema (na kusema), „Ya Allaah!! Basi upesi kaifiche, maana kama unavyomjua mwenzako akiiona lazima ghasia zitakuwepo.“

Lakini kabla sijainua hatua kuificha, Nadya alikuwa kesho tusimamia mlangoni, na kumbe amekwisha yasikia aliyoyasema Mama. Hapo Nadya alisema, „Hapana haja ya kuficha hiyo kalamu, maana watoto wa skuli wamekwisha kuniarifu yote. Lakini Mama, ninakwambia kabisa ujue kwamba ni lazima na miye uninunulie kalamu sawa sawa na hiyo; tena leo hii sasa hivi.“

---

<sup>6</sup> „ (...) nilikuwa ni kama nyota tu mbele ya mbalamwezi (...) “ (Uk. 59).

Na mara Baba aliyekuwa anaingia jikoni kutoka kazini, alimjibu, „Oh! Nadya, kwani hiyo kalamu aliyo nayo Shadya tulimnunulia sisi? Au kapewa kwa jitihada yake? Jitahidi na wewe katika masomo yako, na utapata zawadi nzuri kama hiyo.“

Mama aliruka na kusema, „Ajitahidi vipi tena? Skuli anakwenda kila siku – mvua na jua lake, au unataka agandane na mabuku kama mchwa? Hayo peke yake ni hatari; lakini, Bwana, mimi ninawafahamu vizuri hao walimu, kazi yao ni mapendeleo tu. Watoto wamezaliwa tumbo moja “toka nitoke”, tena vipi ilikuwaje mmoja wamuone hodari, na wa pili ni pocho? Si uongo huo? Lakini haidhuru, mimi mwenyewe nitamnunulia Nadya kalamu, na wao walimu wakae na uhasidi wao – wasimpe cho chote.”

Baba alitikisa kichwa kidogo na akasema, “Mnunulie, lakini ninapenda ajue Nadya kuwa akiwa nayo hiyo kalamu, si kwamba itakuwa sawa uzuri wake kama hiyo ya Shadya, kwani si kuwa amepewa tu, kama unavyofikiri wewe, lakini amepewa kwa sababu anastahiki kupewa – amejitahidi na amefuzu. Na kalamu bila ya shaka si kitu kikubwa, lakini ile sababu aliyopewa yeye ndiyo muhimu, na ndiyo yenye thamani na fahari.”

Mama aliguna akasema, “Ah, Bwana! Hayo siyajui, mimi kumpa nitampa tu.” (Uk. 59-60).

*Als ich sah, dass ich nur Streit zwischen meinen Eltern gebracht hatte, verging mir die Freude. Ich zog mich in mein Zimmer zurück. Mein Vater kam herein, streichelte meine Haare und sagte: „Heute habe ich mich über deinen Erfolg in der Schule und über den Preis sehr gefreut. Morgen werde ich dir ein schönes Geschenk geben.“ Ich dankte meinen Vater dafür. Mein Vater sagte weiter: „Shadya, mein Kind, bleib wie du bist und schätze Bildung hoch. Du ahnst nicht, wie du mir dabei Freude bereitest, wenn ich sehe, dass du fleissig studierst. Ich habe keinen Sohn. Es ist daher mein Wunsch, dass du meine Stelle nehmen wirst, wenn ich gestorben bin. Ich wünsche mir, dass du gut ausgebildet bist und um deine Mutter und um deiner Schwester sorgen wirst.“ Ich schaute meinen Vater in den Augen und sagte: „Inshallah.“ Seine Worte blieben mir auch später in Erinnerung.*

*Ich schätzte meinen Vater mehr und mehr, besonders seine Ideen seinen Charakter. Mein Vater war Arzt und arbeitete in einem kleinen Spital in unserem Dorf. Er liebte seine Arbeit sehr und war nicht auf Geld bedacht. Wir waren nicht reich und lebten auf dem Durchschnittsniveau unserer Gegend. Ich wollte so wie mein Vater Ärztin werden.*

Baba alipata baridi ya kifua alfajiri ile alipokwenda maili mbili kwa miguu na huku mvua kubwa inakunya, kwa ajili gari yake iliharibika, na aliona lazima atoke kumsaidia mzazi. Mama alimkataza sana asende (asiende), lakini baba kabisa hakumsikiliza. Msiba ulikuwa mkubwa sana juu yetu sote nyumbani Baba alipokufa baada ya kumpiga homa ya nimonia muda wa siku tano. Maskini Mama na Nadya hawakujifaa kabisa kwa uchungu; na ijapokuwa na miye nafsi yangu pia nikihisi ninaungua, lakini niliona huu ndio wakati wa kuyathibitisha mapenzi yangu juu ya baba. Nilifahamu kwamba huu ndio wakati wa kuchukua mahala pa Baba yangu na kuwashughulikia Mama na ndugu yangu mdogo. Niliwapoza na nikawapa nyoyo kama nilivyoweza. Hapo nilipiga kifua na kumuomba (kumwomba) Mungu nifaulu katika masomo yangu, ili nipate kuwastarehesha watu wangu kama Baba alivyotuelesha. Ijapokuwa umri wangu hapo ulikuwa ni miaka kumi na nane (minane) tu, lakini nilijihisi kuliko mtu mzima ye yote kwa dhamana nilizojitwika. Kwa

bahati nzuri, Baba alituwachia pesa kidogo za kuweza kuendesha maisha yetu ijapokuwa si kwa raha kubwa kama alipokuwa hai mwenyewe. Aidha ilivyokuwa majirani zetu wote walinufaika sana kwa wema wa Baba yetu, alipokuwa hai, hawakukataa kutusaidia watuonapo tunayo dhiki yo yote. Kwa maisha hayo, tuliweza kuendesha taratibu zote za nyumba kwa wepesi, na ndipo nami nikapata fursa ya kuendelea na masomo yangu.

Jambo kubwa lililokuwa likinishughulisha baada ya kufa Baba ni tabia ya ndugu yangu, Nadya. Alizidi kufanya ayatakayo na kutokuwa na hofu hata kidogo kwa Mama. Mwishowe aliwacha hata kwenda skuli na ikabidi afukuzwe. (Uk. 61).

*Es war nicht so, dass Nadya nicht intelligent war, sondern sie kümmerte sich gar nicht um das Studium. Sie war sogar faul beim Aufstehen und die Mutter glaubte ihr, wenn sie eine Krankheit vortäuschte.*

*Nadya hatte Vertrauen zu mir und manchmal kam sie zu mir, wenn sie Schwierigkeiten hatte. Eines Nachts als ich meine Schulaufgaben machte, rief sie mich zu sich und sagte: „Weiss du Shadya. Ich mag Ahmad nicht mehr, ich möchte, dass Fuad mich heirate.“ Ich bat Nadya mit diesem Blödsinn aufzuhören, aber sie beharrte darauf, dass Fuad sie narrisch mache. Ich wusste, dass jeder Junge sie narrisch macht und bat sie, sich nicht billig zu machen. Nadya wehrte sich dagegen, auf Ahmad zu warten, bis er sein Studium beendet habe, obwohl sie wusste, dass er sie liebt. Sie aber sagte, dass sie ihn nicht liebe, weil er nicht so gross ist wie Rock Hudson und keine breite Schulter hat wie er. Als ich von ihr erfuhr, wer dieser Rock Hudson ist, hielt ich sie für verrückt.*

*Ich versuchte ihr zu erklären, dass nicht nur der Körper, sondern der Charakter eines Mannes mit dem eine Frau ein Leben lang leben werde, wichtig ist. Sie erwiderte, dass es gerade der Charakter von Ahmad ist, der ihr nicht gefällt. Er ist sehr schüchtern und zurückhaltend, sie aber ziehe einen frechen Daraufgänger vor. Sie warf mir vor, dass ich solche Sachen nicht verstehe, weil ich nicht ins Kino gehe. Ich versuchte ihr beizubringen, dass es keinen Sinn hat, sich Träumereien zu ergeben, denn sie werde niemals einen Ehemann bekommen, der einen gesellschaftlichen Status hat, wie Ahmad und dazu ein Gentleman ist wie er. Ich machte sie darauf aufmerksam, wie aufrichtig Ahmad ist. Er hatte von seiner Liebe nie ein Geheimnis gemacht, sondern er hatte seine Liebe ihrer Mutter mitgeteilt und sie versprochen, dass er Nadya heiraten werde. Ahmad hatte ihr nie ein böses Wort gesagt. Er respektierte sie und war nicht wie jene Betrüger, die sie jeden Tag anlügen und dann Böses über sie reden. Ich bat Nadya Ahmad nicht abzuweisen und wünschte ihr eine gute Nacht. Bevor ich zu Bett ging, stand ich dort einige Minuten und schaute zu, wie sie ihren Körper einzog und den Kopfkissen umarmte, als ob sie etwas fürchtete. Sie benahm sich wie ein Kind, obwohl sie bereits das neunzehnte Lebensjahr vollendet hatte.*

*Nadya vergeudete weiterhin ihre Zeit, ohne der Mutter im geringsten bei der Hausarbeit zu helfen. Es fiel ihr nichts gescheitertes ein, als Liebesromane zu lesen und mit ihrer Freundinnen ins Kino zu gehen. Ich hatte inzwischen mein Studium abgeschlossen und die Zulassung zum Medizinstudium bekommen. Die Regierung unterstützte mich finanziell, denn ich hatte die Schule mit guten Erfolg abgeschlossen. Ich war dreiundzwanzig Jahre alt und befand mich im letzten Studienjahr vor der Promotion zum Doktor der Medizin.*



*Eines Tages kurz vor der Regenzeit als ich mit einem Korb voll Bücher müde nach Hause zurückkehrte, wehte ein frischer Wind mir ins Gesicht. Die Landschaft die sich vor meinen Augen ausbreitete war schön und ich spürte im Herzen einen Frieden und eine Fröhlichkeit, so wie ich schon lange nicht mehr gekannt habe.*

Hakika niliuona ulimwengu wa kupendeza mno machoni mwangu, na kuhisi amani na uchangamfu nisiuona siku nyingi. Nilipokuwa nikikaribia nyumbani, nilimuona Nadya, kwa mbali ananipungia mkono, akinikimbilia niliko kwa furaha, na baadaye kunipokea mabuku. Huku akihema, aliniambia, „Shadya, hata sijui nikuhadithie vipi furaha yangu la leo. Kuna jambo kubwa zuri limetokea nyumbani, lakini sikwambii mpaka ulione mwenyewe. Ama leo mambo!” Nami nikamjibu kwa kucheka, “Huwachi mambo yako Nadya? Haya twende tukalion hilo jambo lililokufurahisha.”

Tulipofika nyumbani, niliisikia sauti ya mama inaongea na sauti ya mwanamume. Na kwa nguvu, Nadya alinivuta kuingia chumba cha baraza. Hapo nikamkabili kijana mrefu mwanamume aliye mzuri mno, na ambaye aliyenisimamia aliponiona tu. Nilibabaika pakubwa kama niliyestuka, lakini salama, Mama alinigutuwa aliposema, “Shadya, huyu ndiye Omar, ambaye daima tukisikia habari zake katika barua alizokuwa akiniandikia binti ami yangu. Marehemu Bibi Salwa. Leo yeye ni mgeni wetu, na atakuwepo na sisi kwa siku chache mpaka jahazi yake aliyojia iwe tayari kuondoka.” Tena Mama alimgeukia Omar na kumwambia, “Omar mwanangu, natumai na wewe labda ulipata kusikia kwa Mama yako kama ninaye mtoto aitwae Shadya; basi ndiye huyu.”

Hapo Omar alisema, “Oh! Ndiyo bila ya shaka”. Alinitazama machoni, na kuniambia, baadaye aliongeza kwa kusema, “Hadi nimefurahi kupata fursa hii ya kuweza kukukutana na jamaa zangu ambao miaka mingi nilikuwa nina hamu ya kuwaona.”

Nami nilifurahi kwa maneno hayo, nikasema, “Natumai Omar Instaallah utapitisha wakati wako utakaokuwepo hapa kwa furaha kubwa.”

Mbio mbio Omar alijibu, “Sina shaka nitastarehe sana.”

Kabla ya kuongezeka neno, Nadya aliruka na akamuuliza (akamwuliza), “Kwani Omar jahazi yako itakaa siku ngapi bandarini? Naomba iwe siku nyingi, ya Rabbi”, na tena akanigeukia mimi, “Unasemaje Shadya.”

Omar alicheka kidogo akajibu, “Hakika sina yakini, lakini labda itakaa bandarini muda wa wiki moja tu.”

Nadya alisema, “Ya leit Omar, ungelimaliza mwezi mmoja pamoja na sisi; hadi tungelifurahi.”

“Ya aleit, lakini sikupanga mapema mipango hiyo; na kwa sasa siku zimekwisha – lazima nirudi upesi kwetu kwa ajili ya kazi.”

“Kwani kazi gani unafanya?” Nadya alimuuliza (alimwuliza).

“Ninafanya kazi ya biashara pamoja na wenzangu.”

“Biashara gani hiyo?” Nadya aliendelea kuuliza.

“Biashara ya mazulia.”

“Baba yako yuhai? Na vile vile unao ndugu wanawake?” Nadya hakusita.

“Baba yangu yuhai; mama tu ndiye aliyekufa kama mnavyoyjua. Ama ndugu sina ye yote; ni mimi mtoto pwekee kwa baba.”

Mradi Nadya alimzonga Omar sawa sawa kwa masuala na mazungumzo yasiyo na kisito; na miye na mama kimya tukiwasikiliza. Nilitamani nimkonyeze Nadya, alau apunguze kidogo kusema kwa vile nikitahayari tena, lakini wapi! Hata macho yake sikuyapatia nafsi, kwa jinsi alivyoshughulika na Omar. Hajijui hajitambui! Salama huyo Omar wenyewe alikuwa ni kijana bashashi kwani kamwe hakuonesha (hakuonyesha) kuchoka kwa masuala ya Nadya. (Uk. 63-64).

*Omar verbrachte die ersten vier Tage fast immer daheim bei uns, ausser wenn Nadya ihn mitnahm, um ihn die Stadt zu zeigen. Wir gewöhnten uns schnell an einander. Wir unterhielten uns fröhlich und spielten Karten und andere Spiele.*

*Da ich sonntags keine Vorlesungen hatte, ging ich nach dem Essen zum Strand. Das Wetter war schön, das Meer war still und die Vögel sangen in den Bäumen. Nachdem wir alles ordentlich hingestellt hatten, setzten wir uns auf dem Sand unter den Mangrovenbäumen. Omar schätzte die Gegend sehr und erfreute uns mit Gedichten<sup>7</sup>, die er vortrug. Nach dem Essen ging ich das Geschirr abwaschen und liess die zwei anderen, die Kaffee tranken allein. Omar kam und wollte mir die Arbeit abnehmen<sup>8</sup>, da ich alles allein verrichtete.*

Nikamjibu, „Ahsante sana Omar, lakini hapana kazi yo yote kubwa niliyoifanya. Kwa hivyo, ninakuomba usishike masamli ukaharibu mikono yako. Kakika na sahani zenyewe si nyingi za kuhitajiwa kusaidiwa; sasa hivi nitamaliza kuziosha.“

Lakini Omar hakunisikiliza, bali aliinama na kunisaidia kukosha. Kwa muda, kila mmoja alikuwa kimya, utasema ana fikra za peke yake zinamwenda, na mara nilisikia sauti nzito ya kupowa ya Omar akiniambia, „Shadya, leo ya ngapi nikiitafuta fursa hii ya kuweza kusema na wewe kwa siri; na leo nimeipata, sijui nianze vipi kukwambia ninayotaka (ninayoyataka) uyajue.“

Hakika nilibabaika na kuona haya sana, na labda hata hofu iliingia. Nilitamani nikimbie hapo hapo, na nisiuone tena uso wake; lakini niliona miguu inanicheza, na jasho jembamba linanitoka. Omar aliendelea kusema, „Shadya, ninajua labda umekwisha niogopa (kuniogopa) nilivyokwambia (nilivyokuambia) hayo, lakini toa hofu – mimi sina dhamiri yo yote mbovu juu yako. Shadya, mie ninakupenda, na nimekupenda tangu pale nilipotupa macho yangu juu yako kwa mara ya kwanza. Aidha, katika siku hizi chache tulizokuwa pamoja, nimeyakinisha kwamba hapana tena mwanamke mwengine (mwingine) ambaye (ambaye) atayeniwafiki (atakayeniwafiki) kuwa mke wangu, isipokuwa wewe. Shadya, ninataka kukuoa, lakini kabla sijaleta posa, ninapenda kujua, jee utapenda kuwa mke wangu?“

Bila shaka sikujua nini la kujibu, ila niliona kama niliopo ndani ya ndoto. Yote niliyosikia (niliyoyasikia) niliona hayawezi kuwa. Nilijiuliza nafsi yangu, “Huyu Omar amepotea akili? Kunipenda mimi, na kuacha kumpenda Nadya aliye mzuri? Au anataka kunicheza moyo wangu?“ Lakini utasema alizisoma fikira zangu, kwani alinena, „Ninajuwa (ninajua) labda hunisadiki kama ninakupenda. Lakini Shadya, napenda ufahamu kwamba si ajabu

<sup>7</sup> Ein wesentlicher Aspekt der Swahili-Kultur.

<sup>8</sup> Ein Hinweis die neue Einstellung bei der Swahili-Jugend.

mimi wala mwanamume ye yote kukupenda. Bila ya huo uzuri wako ambao Mungu aliyekutunikia kwa wingi, basi inatosha hiyo tabia na busara uliyo nayo, kumvuta mwanamume ye yote. Shadya, ninajua unaona haya kunijibu lo lote, lakini ulivyonyamaza nimefahamu kwamba hunichukii. Kwa hivyo, kabla ya kumaliza masomo yako, nitaleta posa ili mara tu ukimaliza mtihani nikuoe.” (Uk. 65).

*In diesem Augenblick kam Nadya, fragte uns, woüber wir reden und forderte Omar auf mit ihr zu gehen. Omar stimmte sofort zu und bat sie schnelle zu laufen, damit er sie nachlaufe.*

*Am Abend jenes Tages versuchte ich zu schlafen, aber ich konnte nicht. Die Worte Omars klangen mir in den Ohren. Während ich mich im Bett hin- und herwälzte, kam Nadya herein. Sie wollte herausfinden, was ich mit Omar zu tun hatte und behauptete, dass ich ihn liebe. Ich wehrte mich. Obwohl ich sie bat, schlafen zu gehen, liess sie mich nicht los. Sie wollte unbedingt wissen, was Omar mir dort beim Geschirrwaschen gesagt hatte. Sie fügte hinzu, dass sie nicht erdulden werde, dass Omar und ich allein unter uns sind. Ich sollte Omar ihr überlassen, denn sie liebte ihn. Ich antwortete, dass ich nichts dagegen unternehmen werde, wenn Omar sie heiraten möchte und fragte sie, ob sie Ahmad vergessen hatte. Sie bat mich, Namen wie Ahmad, Fuad und Farouk niemals in der Gegenwart Omars zu erwähnen und sagte, dass dieser Omar für sie mehr bedeute als Omar Shariff, der Kinostar aus Ägypten. Sie hatte aber inzwischen schon erkannt, dass Omar mich liebte und nicht sie.*

*Omar blieb sieben Tage bei uns. Ich hatte aber das Gefühl, dass es ein ganzes Leben gedauert hatte. Obwohl er nie mehr von Liebe sprach, merkte ich, dass er mich liebete. Bei seiner Abreise war ich traurig, versteckte aber meine Trauer, während Nadya laut weinte.*

*Viele Monate gingen vorbei, aber Omar liess nie von sich hören, während ich nach ihm sehnte, tat Nadya, als ob sie ihn veergessen hatte. Eines Tages als ich mich auf die Schlussprüfung vorbereitete, hörte ich jemand die Hausglocke läuten. Nadya öffnete die Türe. Es war der Briefträger. Meine Mutter öffnete den Brief, der an sie, Frau Aliya Mohamed, adressiert war.*

Mpenzi Bibi Aliya Mohamed,

Ama baada ya salamu, nina sharafu kubwa ya kuweza kukuandikia barua hii. Mtoto wangu, Omar, ameniomba baba yake, nilete posa kwa ajili ya binti wako – Nadya Sabri. Tunataraji jawabu kwa upesi.

Mimi hapa,

Kassim bin Ali. (Uk.67).

*Ich hörte Nadyas Namen. Ich hörte meine Mutter sie bitten, das Studium aufzugeben. Ich erkannte nun, dass er mich nicht haben wollte. Mir wurde schlecht, während Nadya den Brief voll Freude küsste, meine Mutter umarmte und im Zimmer herumtanzte. Ich dagegen lief in mein Zimmer hin und weinte. Nach etwa zwei Stunden kam Nadya zu mir, ich aber tat, als ob ich schlafe.*

Nilijidai kulala, kwa sababu sikutaka afahamu yale mahiso yangu, lakini wapi! Nadya hakuniachia ila akaniita, „Shadya, mbona leo umelala na mapema? Husomi? Hebu tafadhali kaa tuzungumze kidogo, na tufurahi kwa posa zangu.“

„Kwa hisani Nadya, zima taa tulale, maana kesho ninataka kuamka alifajiri (alfajiri) nisome; mtihani wangu ni karibu“, nilimjibu.

„Shadya, ninataka kukwambia maneno muhimu, tafadhali nisikilize.“

Hapo nilinyamaza kimya, sikumjibu neno, na Nadya aliendelea kusema kwa sauti isiyokuwa tena ya dhihaka, „Sikiliza, Shadya, posa zilizoletwa leo ninazijua yakini hazikudhamiriwa kuwa ni zangu. Posa hizi zako, na lazima yametokea makaosa katika kuandikwa jina. Unakumbuka alivyokuwa Omar akibabaika na majina yetu? Mara ngapi akikwita (akikuita) wewe Nadya, na mimi kuniita Shadya? Ndugu yangu ninafahamu vizuri kwamba Omar akikupenda wewe wala si mimi, lakini miye ninampenda Omar, na lazima atanioa. Haya yote Mungu amenitengenezea, kwa hivyo hayarudi nyuma. Na ikiwa sasa Omar hanipendi, najua nikishamtia mkononi ndiyo lazima tu atanipenda. Hapo alijongea mbele ya kioo kikubwa cha kabati akipiga nywele zake za mawimbi, refu (nywele ndefu) za kumfika kiunoni. Kisha alisimama akijitazama, naye amekwisha vaa nguo yake ya kulalia nyeupe, nyepesi ya hariri. Alitabasamu kidogo na akaendelea kusema, „Hebu Shadya nitazame Mungu alivyoniumba. Kwa uzuri huu niliotunikwa ndiyo lazima tu nitamtia mkononi mwanamume ye yote nimpendaye, unasemaje? (Uk. 63).

*Ich war völlig ausser mich. Nadya war wirklich schön wie ein Engel. Ihr Körper und ihr Gesicht waren makellos. Obwohl ich mich von Omar verraten fühlte, dachte ich doch, dass Omar von der Schönheit Nadyas angezogen war. Nadya bat mich, das Missverständnis Omars zu vergessen, denn er werde sie lieben lernen und mich vergessen. Ich sollte aber mit meiner Mutter nicht darüber sprechen, sonst könnte ich den Heiratsplan Omars vereiteln. Ich versuchte Nadya zu überreden, dass Omar sie wirklich liebe und unser Namen nicht verwechselt habe.*

*Der Heiratsantrag wurde ohne irgendeinen Widerspruch zugestimmt. Nach einigen Tagen erhielten wir eine Nachricht von Omars Vater, dass wir die Braut zu ihm hinbringen sollten, weil Omar keine Gelegenheit haben werde, zu uns zu kommen. Zwei Monate lang arbeiteten wir fleissig, um alles vorzubereiten, was Nadya für die Trauung und für die Reise benötigte.*

*Ich machte meine Schlussprüfung, ohne irgendwelche innere Teilnahme. Ich war im Gedanken kaum dabei.*

*Am Tag der Abreise verabschiedeten wir uns traurigen Herzens, da wir keinen einzigen Tag getrennt gelebt hatten. Meine Schwester verabschiedete sich von mir mit den Worten: „Shadya, ich bitte dich, vergiss meiner nicht.“<sup>9</sup> Als Nadya vom Schiff her mir zum Abschied zuwinkte, wusste ich, dass ich Omar niemals heiraten werde, obwohl ich ihn nicht vergessen konnte. Das war mein Schicksal.*

---

<sup>9</sup> „Shadya, ninakuomba usinisahau.“ (Uk. 69). „Usinisahau“, „Forget me not“ ist die Überschrift dieses Kurzromans und auch den Namen einer Blume.

Maskini Omar! Aliniletea barua baada ya kuonana tu na Nadya. Nilifungua barua hiyo na huku moyo unaniambia: niichane wala<sup>10</sup> nisiisome, lakini wapi! Mwishowe sikuweza, ila niliyasoma mbio mbio yafuatayo:

“Shadya mpenzi wangu,  
Ninaona haya na aibu kufanya makosa niliyoyakosa. Shadya, ni wewe nikupendaye kama unavyojua, na ndiye wewe ninayetaka kukuo; siye Nadya.  
Nisamehe na unihurumie nisiadhibike milele kwa ajili ya makosa ya kuisahau hiyo herufi moja ya mwanzo ya jina lako.  
Shadya macho yangu, kama unanipenda ijapokuwa kidogo tu, tafadhali ninataka kukuo. Nijibu kwa upesi.  
Wako wa daima,  
Omar.”

Nilijibu barua hiyo kwa haraka na kwa kujilazimisha. Nilijua sina la kufanya lo lote jingine kwa sasa ila lazima nimsahau Omar katika maisha yangu, nikipenda nisipende; ni hii ndiyo fursa yangu nzuri. Nilimuandikia na machozi yananitoka:

“Mpenzi Omar,  
Ninasikitika kukwambia kwamba sitaki kuolewa na wewe kwani sijapata kukupenda hata siku moja. Nadya ndiye akupendaye, na kwa hivyo ninakuomba usimvunje moyo, na ukamtahayarisha na ulimwengu.”  
Shadya.”

Ni kweli sikuweza kabisa kumla kinyume ndugu yangu; na kama mwanzo nilivyompa ahadi kwamba nitamsaidia aolewe na Omar, bila ya shaka kwa sasa tena sikuwa nina moyo wa kuweza kumvunja furaha na matumaini yake. Kwa hivyo Omar hakuwa na hila ila ndiyo amuo tu bi-arusi aliepelekwa (aliyepelekwa), akipenda asipende. (Uk. 70).

*Die Briefe Nadyas betrübten meine Mutter, denn sie zeigten kein Zeichen der Freude. Nadya sagte uns, dass sie sich bemühte, das neue Leben gut zu gestalten. Eines Tages als ich vom Einkaufen zurückkam, fragte mich meine Mutter bestürzt, warum ich ihr, den Brief Omars nicht gezeigt hatte. Sie hatte ihn gefunden und gelesen. Sie machte mir Vorwürfe, dass ich Nadya mit einem Mann heiraten liess, der sie nicht liebte. Ich hatte ihr mitgeteilt, dass Nadya alles gewusst hatte. Sie wusste, dass Omar mich liebte, sie wusste auch, dass der Heiratsantrag mir galt und nicht ihr. Meine Mutter gab sich aber nicht zufrieden und rügte mich, dass ich so etwas zugelassen hatte. Meine Mutter quälte sich innerlich, wurde krank, der Blutdruck stieg und innerhalb einer kurzen Zeitspanne von zwei Wochern alterte sie schnell.*

*An jenem Tag an dem ich das Ergebnis meiner Prüfung erhielt, kam ich nach Hause und wollte meiner Mutter behutsam mitteilen, dass ich durchgefallen war. Ich wurde jedoch vom Hausarzt vor dem Eingang des Hauses aufgehalten. Sorgfältig und langsam sagte er mir, dass er sein Bestes getan hatte, aber ihre Gesundheit sich verschlechtert hatte.*

---

<sup>10</sup> „Wala“ bedeutet „weder noch“ und wird so gebraucht: „Nilihisi wala nisiifungue barua wala nisiisome.“

„Shadya, nasikitika sana. Nimejaribu kama niwezavyo kumsaidia Mama yako, bali nimeshindwa, Bwana Mungu anamtaka kiumbe chake.“ Hapo sikumjibu neno ila nilimkimbilia chumbani kwa Mama yangu na kupiga magoti karibu yake, Mama aliponiona, uso wake ulimkunjuka kidogo, akashuka pumzi na kuniambia kwa sauti dhaifu:

„Shadya mwanangu umefika? Sasa niradhi nikifa, kwani alau mtoto wangu mmoja yupo mbele yangu. Shadya Mama, buriyani (buriani). Nisameheni wanangu kwa yote niliyoyakosa. Najua ni makosa yangu leo kuadhibika na maisha. Kwani ingelikuwa nimekuleeni kwa vizuri kwa kukuonyesheni mapenzi sawasawa bila ya kumpa kichwa mmojawapo au kumtia unyonge wa pili, leo musingelikuwa na maisha ya majonzi nyote wawili.”

Tena aliendelea kusema:

“Lakini Shadya, ninakuomba ujue kuwa si kwamba hasa nilikuwa nikikupenda kasoro kuliko Nadya, ila nilikuwa ni Mama mjinga tu nisiyejua kulea. Nisamehe mwanangu, Mungu atakupa furaha na mafanikio ya maisha, kwani bila ya shaka – ‘Mtenda zema(?) laazima kulipa mema.’ Shadya, ninakupa radhi yangu na ninakuomba usubiri.”

Baada ya kuhangaika kwa kitambo cha nusu saa Mama yangu mpenzi, alimalizika. (Uk. 72).

*An diesem einen Tag trafen mich zwei Schläge. Ich wollte nicht mehr in diesem Haus wohnen. Sofort nach der Trauerfeier nahm ich einige wichtige Sachen mit und verließ das Haus, ohne zu wissen, wohin ich gehen wollte. Ich ging zum Strand und setze mich dort nieder.*

„Hapo moyo uliniambia, „Bora jitose baharini ufe, kuliko kuishi na mateso haya.“ (Uk. 73).

*Ich war so müde und erschöpft, dass ich bald einschlief. Ich weiss nicht, wie lange ich dort lag. Ich erwachte plötzlich, als jemand mich stiess und mich aufforderte aufzustehen. Ich öffnete meine Augen und sah, dass es dämmerte. Ich sah, dass das Wasser des Ozeans nahe bei meinen Füßen gekommen war. Ein Mann stand vor mir und half mir aufzustehen. Er brachte mich in sein Haus, liess mich vor einem Arzt untersuchen und zusammen mit seiner Ehefrau sorgte er für mich. Beide wollten mehr über mich wissen und ich erzählte ihnen alles, was mich dazu geführt hatte, mein Elternhaus zu verlassen. Sie baten mich, bei ihnen zu wohnen und auf die Prüfung vorzubereiten. Ich sagte gerne zu. Herr Is-haak und Bi. Aisha lebten gut in einem grossen Haus mit sechs Dienern. Ich hatte ein Zimmer, das luxuriös ausgestattet war, zur Eigenbenützung. Das Haus stand nahe beim Ozean.*

Kwa bahati niliweza kuona wema na utajiri nisyopata kuuona tangu kuzaliwa kwangu. Bwana Is-haak akiishi kama mfalme nyumbani kwake, pia akipenda na kuenziwa ajabu na wote waliokuwa chini yake. Alikuwa mashuhuri kwa ukarimu, utajiri na umahashamu wa kupigwa mfano, na si yetu tu bali ndivyo ulivyokuwa ukoo wake wote. Ni kawaida ya asili na asili kwa kila Ijumaa, baada ya sala ya aduhuri, nyumba hii hujaliwa na maskini na wahitaji wakapewa haja zao bila ya kusailiwa sana. Bwana Is-haak hakujua kabisa kumsahau ye yote aliye chini yake hasa siku ya Sikukuu. Hutoa mazawadi yakaenea kwa kila mmoja hata kwa watoto walio matumboni. Maskini Bibi Aisha alikuwa akiishi upweke

tangu aliposafiri mtoto wao mwanamume ambaye ni mmoja tu. Alinihadithia kwamba amekwenda Ulaya kusomea uwakili. Lakini ilivyokuwa baadaye amenipata mimi aliniambia, „Ninashukuru, moyo wangu umekunjuka sana sasa na hadi unanichangamsha.“

Yeye na mumewe walijaribu kama wawezavyo kunistarehesha. Hapana hata moja lililokuwa nikilitamani wasinifanyie. Mara tu walipotambua kwamba bado nilikuwa nina mapenzi ya kuwa dakitari, walinitia hima na kunishikilia nijaribu tena kuchukua mtihani. Na kwa bahati nzuri mara hili nilifuzu. Hapo tena bila ya kukawia, nilisitukia Bwana Is-haak amenikabidhi funguo za kufungulia Hospitali ndogo yangu mwenyewe. Nilipokuwa nikibabaika sijui vipi nimshukuru alinituliza na kuniambia, “Baba ye yote anapofurahiswa na mwanawe naye hutunza.”

Hadi nilipenda sana hospitali yangu hiyo, ilivyojengwa kwa kidesturi na kutiwa vyombo vya kufanyia kazi ambavyo vyote vipya na vya kisasa kabisa. Nilianza kazi kwa hamu kubwa na kwa kitambo cha mwaka mmoja tu, nilijiona nimegeuka kuwa Shadya mwingine kabisa, siye yule Shadya aliyekaribia kujiua nafsi yake siku ile pwani. Nilihisi maisha yangu haya mapya kwa kupitisha kila dakika ya uhai wangu kwa ukamilimu na kwa raghba ya kupenda kuishi zaidi na zaidi. Furaha yangu ilikuwa inatosha pale ninapojiona ninaweza kuwatumikia watoto, vizee, wanawake na pia wanaume wagonjwa ambao wanahitajia msaada wangu kuwatibu. Nilimshukuru Mola wangu kunijaalia ndoto yangu hii kuwa ni kweli na matumaini yangu hayakuwa yamepotea na upepo. (Uk. 74).

*Ich freute mich nun meine eigene Parxis zu haben. Ich wohnte noch bei der gleichen Familie und wünschte mir, dass ich irgendwie ihre Güte vergelten könnte. Meine zwei Pflegeeltern sprachen oft von ihrem Sohn Nabil. Eines Tages kam Bibi Aisha zu mir mit der Nachricht, dass er bald heimkehren würde. Die Vorbereitungen für den Empfang waren umfangreich. Das ganze Haus wurde ausgemalt, neue Möbelstücke wurden in das Zimmer Nabils gebracht und neue Rosensträucher wurden in den Garten gepflanzt. Nabil wurde mit einer grossen Festfeier empfangen.*

*Als Sheikh Is-haak mich zum ersten Mal Nabil vorstellte, gefiel er mir. Ich wollte aber nicht lange dort bleiben und erfand eine Ausrede, um sofort hinauszugehen. Obwohl ich gerne von ihm fern geblieben wäre, liess er mich nicht in Ruhe. Er suchte immer nach einer Gelegenheit, mich zu nähren und sich mit mir zu befreunden, so dass es mir schwierig wurde, ihn zu vermeiden. Er pflegte es, mich in meiner Praxis zu besuchen und mir zu helfen, damit er mich nach Arbeitsschluss nach Hause begleiten konnte. Allmählich gewöhnte ich mich an ihm und begleitete ihn, wenn er die Plantagen seines Vaters besuchte, falls ich dienstfrei hatte. Er war ein fröhlicher Mensch und liebte es zu scherzen und zu lachen.*

*Eines Tages lud er mich ein, eine der Plantagen seines Vaters zu besuchen, denn er hatte dort dienstlich etwas zu tun. Als wir dort ankamen, sprach er mit dem Dienstvorsteher und bat mich vorzugehen. Ich ritt weiter auf meinem Pferd, aber kaum war ich einige Schritte geritten, rief mich jemand laut. Als ich mich umdrehte, sah ich Nabil auf dem Boden vor seinem Pferd liegen. Er zeigte Zeichen des Schmerzes, liess mich aber nicht von ihm behandeln. Er wollte unbedingt auf meinem Pferd sitzen und von mir nach Hause gebracht werden. Ich hatte keine andere Wahl, als seinen Befehl zu folgen. Während wir nach Hause*

*ritten, hielt er an mich fest und umarmte mich an meiner Brust. Ich war in Bedrängnis und bat ihn höflich, mich nicht zu fassen. Aber er blieb bei seinem Vorhaben.*

*Zuhause angekommen, lag er auf seinem Bett und bat mich, seinen Fuss zu untersuchen. Als ich aber an die Arbeit gehen wollte, brach er in lautes Lachen aus. Ich dachte, dass er aus Schmerzen ausser Sinnen war. Ich sah kein Zeichen der Verletzung. Das machte mich wütend und ich verliess das Zimmer sofort. Am folgenden Tag bat Nabil mich um Verzeihung und versprach, dass er solche Scherze nie mehr wiederholen werde. Aber ich kam nicht mehr zur Ruhe und vermied ihn eine Ganze Wochen lang.*

*Eines Tages als ich im Garten Blumen pflückte, legte mir jemand seine Hand auf meine Augen. Ich wusste, wer es war und bat ihn, seine Hände zu entfernen. Er dagegen sagte mir, dass er so gerne hörte, wie ich seinen Namen aussprach und bat mich, es zu wiederholen. Ich schob ihn weg und ersuchte ihn mit solchen Spässen aufzuhören. Er aber drängte mich mit der Bitte, ihn zu heiraten. Ich antwortete, dass ich niemals heiraten werde, weder ihn noch sonst jemanden. Ich fügte hinzu, dass er für mich nur wie ein Bruder war. Als er mich mit seinem Heiratsantrag weiterhin drängte, sagte ich ganz fest, dass ich die Absicht zu heiraten schon aufgegeben habe. Nabil ging weg und machte keine Annäherungsversuche mehr. Ich aber fühlte mich einsam, denn Nabil hatte sich von mir distanziert. Wir trafen uns nur bei Mahlzeiten im Familienkreis.*

Siku moja baada ya kula chakula cha usiku, Bibi Asiha alinizuia nisiondoke na akaniita faragha chumbani kwake, hapo alianza kuniambia, „Shadya mwanagu, nimekwita (nimekuita) kukuambia kwamba Nabil anaondoka, na si kwamba anaondoka kwa kutembea bali anaondoka kwa kuuhama mji hasa.“ Hapo alisita kidogo, tena akaendelea, „Shadya unajua muondoko (mwondoko) wa Nabil wa namna hiyo utaniathiri vipi? Nitaumia. Shadya, mimi sasa ni kizee na kufarikiana tena na mwanangu ambaye miaka mitano nilikuwa nikingojea awe karibu yangu, sasa akiondoka siwezu kuchukua. Shadya, ninakuomba ikiwa inamkinika, unisaidie nimalize maisha yangu kwa amani, tafadhali nizuilie Nabil kwa kukubali uolewe naye. Hapo nilistuka kwa maneno yake hayo na nikamwambia, „Lakini vipi niolewe naye na mimi simtaki?“ Akaendelea kusema, „Shadya mwanangu, Nabil anakupenda na anataka kukuoa, na wewe pia unampenda ijapokuwa mdomoni unasema humpendi na unajaribu kujiaminisha nafsi yako kwa hayo, Shadya usiharibu mustakabali wako kwa ajili ya jinamizi la usingizini. Starehe na uhai wako, usahau maovu yaliyokufika. Bila shaka kwa Nabil hayatakutokelea tena wala usiogope.“

Sijui kwa nini nilihisi machozi yanailengalenga nikatamani nilale juu ya bega la Bibi Aisha, lakini niliinuka na kabla sijaondoka aliniambia, „Shadya, nenda kafikiri uzuri (wa) maneno yangu, usifanye haraka ukaharibu maisha yako mara ya pili.“

Muda wa siku tatu niliyawaza ya Bibi Aisha ambayo hatimaye sikuweza kukataa na kuona kwamba labda ni maneno yaliyojaa kweli tupu. Lakini kwa jinsi nilivyojaribu mpaka dakika ya mwisho kutoyaamini nilijidanganya nafsi yangu kwa kujiambia, „Basi hata ikiwa simpendi Nabil siolewi naye kwa ajili ya mapenzi, lakini jee (je) pia siolewi kwa ajili ya kulipa ihsani ya wazee wake? Hii ndiyo fursa yangu ya kuwalipa wema wazee hawa



wazuri, ni bora nijitoe muhanga<sup>11</sup> nafsi yangu kwa kuridhi niolewe na mtoto wao alau asiwakimbie.“ Kwa hiyo niliolewa an Nabil. (Uk. 77-78).

*Die Hochzeit war sehr feierlich und mehr als 2000 Gäste waren eingeladen. Nach der Hochzeit gingen wir auf eine Insel, die unbewohnt war, abgesehen von drei Personen die dort arbeiteten. Wir nahmen keinen Diener und keine Dienerin mit. Ich freute mich, Nabil näher kennen zu lernen.*

*Wir kamen zurück und lebten weiterhin in Nabils Elternhaus. Eines frühmorgens als es dämmerte, während Nabil noch schlief, nahm ich mein altes Photoalbum, setzte mich und weinte, denn an diesem Tag wurde Nadya 25 Jahre alt und somit erwachsen. Nabil, der inzwischen wach war, lachte mich aus, weil ich über meine Kindheitserinnerungen weinte. Er schlug vor, entweder Nadya gemeinsam zu besuchen oder ihr die Reise hieher zu finanzieren. Während wir noch miteinander plauderten, kündigte unsere Dienerin Amina einen Besuch an, nämlich ein Mann mit einem dreijährigem Kind.*

Bwana mgeni baada ya kuniambia alijijulisha kwangu kwa kuniambia, „mimi ni Suleiman, mjumbe niliyepewa huyu mtoto na hii barua, niwasilishe mwako.“

„Umepewa na nani?“ Nilimwuliza.

Akanijibu, „Nimekabidishwa na rafiki yangu mmoja ambaye akijua kuwa nitamtembelea miji hii katika safari zangu. Hasa alinipa anuwani (anwani) ya kijiji kingine, bali nilipokwenda huko watu wa mtaani ndio walionifahamisha kwamba sasa umehamia hapa.“

Nilimshukuru kwa taabu aliyochukua tena ndio nikaipokea barua kwa mastaaabu makubwa na hamu ya kujua inakotoka. Lakini mara ndani ya bahasha, niliweza kuona hati nizijuazo vyema ambazo siwezi kuzisahau maisha yangu. Bila shaka ni hati za Nadya.

Barua hiyo ilisema hivi:

“Shadya, ndugu yangu mpenzi,

Ilivyokuwa leo dakitari amekwisha niambia kwamba siku zangu za kuishi zilizonibakilia ni chache kabisa, basi ndio nimeona bora nikuandikie barua hii ya mwisho ya maagano. Barua ambayo nitakayoamrisha uletwe baada ya mimi kuwa sipo tena duniani. Shadya najua kwamba kukuomba msamaha ni ombi kubwa sana ambalo sistahiki kupewa na wala sithubutu kukulaumu. Lakini Shadya, kabla sijaenda kaburini ninapenda ujue kwamba nakufa na huku nakutaja jina lako. (...).

Nimekupokonya Omar, lakini na miye pia sikumpata. Kwa miaka miwili niliyokaa naye sikuona (wala) furaha wala raha yo yote ile kwake, ambayo niliyoitumaini. Mwishowe kati ya magomvi yetu ambayo yasiyokwisha, Omar aliniambia maneno ambayo maisha nimeyakumbuka, nayo ni, “Nadya nilipokuoa si kwamba nilikupenda bali nilivyolazimika nilidhamiria nikupende mke wangu. Lakini mpaka sasa nimefahamu kuwa siwezi kabisa kufuzu, kwani mapenzi si kupenda tu bali pia ni na kupendwa. Na wewe Nadya,

---

<sup>11</sup> Dieser Begriff kommt auch in Kiu von Mohamed Suleiman Mohamed aus Sansibar vor. Dort nennt Bahati sich selbst „muhanga“.

ninasikitika kukwambia kwamba hilo kwako ni mustahili kupatikana. Wewe ni ujipendaye nafsi yako tu, na huwezi kabisa kumpenda ye yote mwingine (mwingine), Kwaheri.”

Bila ya shaka, niliona moto usoni mwangu, na kwa uchungu na ghadabu niliyokuwa nayo nilimchukia hapo hapo Omar, nikatamani nimue dakika hiyo hiyo. Kwa hivyo sikuweza kustahamili ila nilivurumisha gilasi ya maji ya machungwa niliyokuwa nayo mkononi, nikamtupia kwa nguvu usoni mwake. Matokeo, Omar hakusalimika kabisa maskini! Ameathiriwa jicho lake ambalo halitoona (halitaona) tena maisha. Aaah! Shadya, huo ndio mwisho wa Omar wangu kwangu. Amenisamehe na miye pia nimemsamehe kwa kunikimbia pamoja na mwanawe, ambaye daima hakuwa na hakika kwamba yakini ni wake. Simjui Omar alipo hii leo. Nimesikia kwamba amekwisha oa (kuoa) na Inshallah ninamwombea awe amekwisha sahau maisha maovu niliyomkutisha.

Shadya, ijapokuwa dakitari labda hajafahamu, lakini miye mwenyewe ninajua kwamba dhiki na majuto ndiyo sababu ya maradhi yangu haya yote. Dada yangu niliyekutegemea daima, tafadhali sana nipokelee Salwa (Eigenname) kwani sina mwinginewe (mwingine) wa kumwachia. Ninaamini kwamba utampenda (Salva) na utasahau uovu wa Mama (Nadya) yake. Kwaheri.

Nduguyo akupendaye,  
Nadya.”

*Nadya hatte mir ihre Tochter Salwa übergeben. Der Bote hatte mir das Kind hierher gebracht.*

Pamoja na donge la uchungu moyoni, taratibu niliupapasa uso wake kwa kuukumbuka ule niujuao sana, na moyoni nikasema, „Huu ndio uso wa yule mtoto aliyekuwa pamoja nami udogoni, tukicheza na kucheka kwa furaha, pale bustanini nyumbani, na huku Mama na Baba wakituangalia kwa macho yao yaliyojaa mapenzi.“

Salwa alikuwa kainama kama anionaye haya na huku anachezea kitu ambacho alichokivaa mkononi mwake. Nilipokitazama nilikiona kwaamba ni ile ile bangili ya fedha niliyompa Mama yake hapo udogoni ambayo yenye maandishi „Usinisahau“.

*Ich umarmte Salwa und sprach:*

„Oh! Nadya umezaliwa tena na kwangu miye hujafa, kwani ndiyo kwanza umerejea katika maisha yangu.“

Tamati

